



NASAHU KWA WANAOUNGA NA WASIOUNGA MKONO MAULIDI



Tukiwa katika mwezi wa Rabi ul Awal (Mfunguo sita) aliozaliwa Mtume wetu mtukufu (SAAW). Hapana shaka sote twajua uwepo wa mizozo na mivutano isiyo yalazima baina ya baadhi Waislamu kuhusu sherehe ya Maulidi.

Si lengo la maandishi haya kuone-sha nani yupo sahihi na nani hayupo sahihi kuhusu suala la maulidi baina ya pande mbili. Saba-bu ni kwamba hili ni jambo lenye kukubali ikhtilafu, hivyo, tuta-waachia watu na misimamo yao.

Sababu za ikhtilafu ni kuwepo tofauti katika uwezo wa kufahamu nususi za kisheria na ni jambo lipo na pia limedokezewa katika Quran Tukufu:

هُوَ الَّذِي أَنْزَلَ عَلَيْكَ الْكِتَابَ مِنْهُ آيَاتٌ مُحْكَمَاتٌ هُنَّ أُمُّ الْكِتَابِ وَأُخَرُ مُتَشَابِهَاتٌ

“Yeye Peke Yake Ndiye Ambaye

Aliyekuteremshia Qur’ani ambayo katika hiyo kuna aya zenye maana yaliyo wazi; hizo ndizo msingi wa Kitabu (ambao unategemewa ikitokea chochote kinachohalifiana nao kinarudishwa na kuoanishwa nazo.) Na katika hiyo (Quran) kuna aya zingine mutashābihāt: (zinazoleta na kubeba zaidi ya maana moja (haiwezekani kujua maana iliyokusudiwa, isipokuwa kwa kuziambatanisha na muḥkam:))”

(Surat Imran: 7)

Hivyo, kudai kwaamba hakuna ikhtilafu katika jambo la mawlid ni kuleta ikhtilafu kubwa kuliko hiyo inayopingwa.

Jambo la kusikitisha katika qadhia ya ikhtilafu ni uwepo wa matumizi mabaya ya ikhtilafu, imma kwa nia mbaya au kwa bahati mbaya. Kama vile kuzuwa vurugu baina ya Umma kwa jambo lenye kukubali ikhtilafu, au kuingiza kwenye ikhtilafu mambo ambayo hayakubali ikhtilafu kwa kutumia mlango wa uwepo

Inaendelea ...Uk. 3

AFRICA50 NI MKONO WA UKOLONI KATIKA UBORA WAKE



Tarehe 5–6 Agosti 2026, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliandaa mkutano wa Jukwaa la Miundombinu kwa Africa (AFRICA50) pamoja na Mkutano Mkuu wa Wadau wa Africa50. Mkutano huo wa kimataifa ulifanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), ukiwakutanisha wakuu wa nchi mbalimbali, wawekezaji binafsi, waendelezaji wa Miradi, wataalamu wa miundombinu na wataalamu wa Fedha kwa lengo la kujadili mabadiliko na maendeleo ya kiuchumi barani Afrika.

Africa50, ambayo ni jukwaa la uwekezaji katika miundombinu kwa umajmui wa Afrika lilianzishwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika pamoja na mataifa ya Afrika mwaka 2014, linalenga kuharakisha utekelezaji wa miradi ya miundombinu na kuifanya miradi hiyo iweze kuvutia ufadhili wa kifedha. Aidha, linalenga kusaidia kuziba pengo la ufadhili

Inaendelea Uk. 6

Yaliyomo :

- ♦ Tahriri—Mazazi ya Mtume Yawe Chachu..... 2
- ♦ Ubalozi wa Marekani Afghanistan 2
- ♦ Jee inafaa kunufaika na Najsi.....4
- ♦ Kupunguza Idadi ya watu 5

**BALOZI ZA MAREKANI NI VITUO VYA UJASUSI NA UGOMVI;
KUIALIKA MAREKANI
KUFUNGUA UBALOZI WAKE TENA NCHINI AFGHANISTAN
NI USALITI KWA MIHANGA YA
UMMAH WA KIISLAMU NA TUSI KWA DAMU YA MASHAHIDI**



Katika mahojiano ya hivi karibuni na The New York Times jijini Kabul, waziri wa mambo ya nje wa Afghanistan alialika rasmi Marekani kufungua tena ubalozi wake na kuwekeza katika sekta za miundombinu na madini za Afghanistan, akisema: *"Tunachukulia sura ya vita kuwa imefikia mwisho, na kuanzia sasa, tunataka uhusiano unao- tegemea heshima ya pande zote na mwanzo wa sura mpya ya ushirikiano chanya."*

Kuzungumzia "mwisho wa sura ya vita" na dola ambayo inashiriki katika vita vipana na vya uadui dhidi ya Ummah wa Kiislamu ni kosa la kimkakati na kitendo cha kufumbia macho ukweli usiopingika. Marekani ni kiongozi wa ukafiri wa kima-taifa na adui mkuu wa Waislamu. Ingawa Marekani kwa sasa haipigani vita vya kijeshi nchini Afghanistan, mtazamo unaozingatia Ummah unaweza wazi kwamba Amerika, kwa wakati huu, inapigana na Waislamu katika nyanja kadhaa na iko mstari wa mbele katika migogoro hiyo. Marekani inacheza dori katika vita vya Yemen na mgogoro wa umwagaji damu nchini Sudan;

inawapa Mayahudi msaada usio na kikomo wa kijeshi, kisiasa, na silaha katika mauaji ya halaiki ya watu wa Palestina na Lebanon; Pia imefuata sera za shinikizo, vikwazo, na mapambano dhidi ya Iran. Pamoja na maendeleo haya, inaunga mkono sera za serikali ya India za uvamizi na ukandamizaji dhidi ya Waislamu, kuongezeka kwa taharuki na Pakistan dhidi ya Afghanistan, na kuwekwa kwa mashinikizo la kisiasa, kiuchumi, na usalama dhidi ya Afghanistan.

Katika mizani ya Uislamu, kipi-mo cha *al-walā* wa *al-barā* hakimuliwi na mipaka ya kikoloni au fahamu za kitaifa. Uadui dhidi ya Marekani umejikita katika mapambano ya kimsingi kati ya ukafiri na Uislamu. Kupuuza uhalifu wa dola hii ya kikoloni katika ardhi za Waislamu kwa kisingizio cha maslahi ya kitaifa ni kuondoka kutoka kwa kanuni za imani ya Kiislamu na kupuuza mtazamo mmoja wa kisiasa wa Uislamu. Zaidi ya hayo, uadui wa Amerika dhidi ya Afghanistan haujawahi kuisha. Kutokuwepo uwepo wa kijeshi wa Marekani hakumaanishi kwamba vita vimekwisha au kwamba amani imeanzishwa; badala yake, Marekani imebadilisha mbinu yake kutoka vita vya moja kwa moja vya kijeshi hadi shinikizo la kiuchumi na kisiasa na operesheni za kijasusi.

Inaendelea uk 7

MAZAZI YA MTUME YAWA CHACHU KWA UMMAH

Mwezi wa Rabiul-awal ndio ali-ozaliwa Mtume SAAW, vivo hivyo mwezi wa Septemba kama huu mwaka 643 ndipo Khilafah ya Umar ibn Khattab chini ya Jemadari wa Kiislamu Khalid Ibn Walid ilikamilisha fathi ya mji wa Damascus kutoka kwa Warumi (Byzantine).

Khalifah Umar na Khalid ibn Walid (ra) ni wanaume wachache katika wengi alio-waandaa Mtume SAAW kuhifadhi Khilafah na kubeba majukumu yake, na waliyabeba kwa utiifu mkubwa ambapo leo Umma unakula matunda ya kuenea Uislamu mashariki na magharibi.

Ni wajibu Umma wetu katika kuyakumbuka mazazi ya Mtume SAAW tuone namna alivyofanya kazi kubwa ya kufinyanga Waislamu majasiri wa kujitolea ambao hawakusita inapokuja ajenda nyeti ya kuunusuru Uislamu. Leo Waislamu tusimalizie kukumbuka mazazi ya Mtume SAAW bila ya kuchukua msimamo thabiti juu wa dini yetu.

Kumbukumbu ya mazazi ya Mtume SAAW itusukume kubeba msimamo wa Uislamu kwa hali na mali kwa kurejesha tena dKhilafah inayopaswa kuanzia nchi kubwa za Waislamu na kuenea kila mahala.

Mhariri

01 Rabiul Awwal 1448 Hijria

Septemba 2026 M

jukwalakhilafah@gmail.com

wa ikhtilafu.

Lengo la makala hii ni kuonesha namna sherehe za mazazi ya Mtume SAAW yanavyobebwa vibaya kwa pande zote mbili, wanaounga mkono na wanaopinga:

1. Kwa Wanaounga mkono sherehe za mazazi ya Mtume SAAW:

a. Kutanguliza mambo ya mubaha kuliko ya wajibu. Mfano, kutokusanya nguvu na mali kwa ajili walimu wa madrasa na kuboresha madrasa lakini kutumia nguvu kubwa na mali nyingi kwenye sherehe za maulidi.

Kwani uwezekano wa kufanya sherehe isiyo na gharama kubwa tena ya muda mfupi ni jambo linawezekana, kama kutoandaa chakula nk. na huenda wakapata picha halisi ya wanaohudhuria kwa mapenzi ya Mtume SAAW na wanaohudhuria kwa sababu zao.

b. Baadhi ya sherehe hizo za maulid kutojali ratiba za swala na ibada nyengine. Hili ndio jambo baya zaidi, vipi tumo katika kumsifia Mtume SAAW kuchukue nafasi, kuliko kutekeleza maagizo aliyokuja nayo Mtume SAAW?

c. Jukwaa la mazazi ya Mtume SAAW aliyekuja kupambana na ukafiri kutumiwa kukuza agenda za kikafiri kama vyama vya siasa vya kikafiri vinavyotangaza wazi kwamba itikadi yake ni kutomtambua Allah Taala katika nyanja za maisha, yaani wanakusudia haki na milki ya Allah Taala ni ndani ya kuta nne za majengo ya ibada tu.

Hakika hii ni aibu sana na ni kesi kubwa Siku ya Qiyama kutumika jukwaa la Mtume SAAW kwa matumizi dhidi ya Mtume SAAW.

Katika watu waliomtesa Mtume SAAW ndani ya Makka ni akina

Abuu Jahali ambao nao walikuwa na itikadi inayofanana na leo kwamba Mungu Muumba asihusike katika maisha yao ya siasa, uchumi, utawala, jamii, adhabu za wahalifu, haki na wajibu nk.

Basi vipi watu walioshikilia itikadi ya Abuu Jahali ima kwa kujua au kutojua (kwani baadhi yao bado ni Waislamu na sio kwamba wameritadi) wapewe nafasi ya kunadi sera zao katika jukwaa la Mtume SAAW au kuombewa dua waweze kuendeleza mifumo yao isiyo na dini?

d. Majukwaa kama haya ya maulidi yanafuatiliwa na Umma wa Kiislamu na kuyategea masikio, basi katika majukwaa kama haya kutozungumzwa mada zenye kuhuisha fikra, ari, na hamu kwa Umma wa Kiislamu kuwa pamoja pasina kujali ikhtilafu zetu za rangi, kabila, madhihab, au hii mipaka bandia iliyochorwa na wakoloni, ni matumizi mabaya ya majukwaa hayo ya mwezi kama huu wa mazazi ya Mtume SAAW.

Kwa bahati mbaya sherehe na majukwaa haya kuanzia mara nyingi mwanzo mpaka mwisho hakuna hata dua ya kuwaombea Waislamu wanaodhulumiwa kama mauaji ya mayahudi ndani ya Gaza, Kashmiri, Burma, Turkistan Mashariki nk. Lakini bada la yake utasikia dua za kuwaaombea wanasiasa ambao hawana haja na dua hizo bali ni kujipendekeza tu, kwani karibu kila mwanasiasa ana mganga wake, je mwenye mganga ana haja na dua? Na vipi mtu

anaombewa dua apate kendeleva maasi? Kwani siasa na hukmu zisizokuwa za Kiislamu ni maasi ya wazi, na hili halina ikhtilafu kwa wasomi wote wa Kiislamu.

e. Majukwaa haya ya mazazi ya Mtume SAAW hutumika kurusha vijembe kwa makundi yenye kupinga sherehe hizi kuliko kuelimisha Umma, kwani wapingao sherehe hizi hoja zao zinajulikana, na tayari zimeshapingwa. Na pia waungaji mkono sherehe za maulidi na wao hoja zao zinajuulikana. Sasa kwanini kusitumike majukwaa haya kuamsha Umma badala ya mivutano?

f. Ukweli halisi wa faida ya kumbukumbu ya uzawa wa Mtume SAAW haufafanuliwi vizuri na kwa kina. Bali kinachodhihirika ni kusemwa kipande, na kipande kufichwa au kuachwa kwa bahati mbaya. Bali ukweli hasa uzawa wa Mtume SAAW ilikuwa ni kuchomoza nuru mpya ya mfumo wa Uislamu, dini iliyokusanya roho na siasa. Yaani ni ujio wa mfumo wa maisha wenye nidhamu ya utawala, siasa, uchumi, jamii nk.

Na hii ndio sababu ya uadui wa Makuraishi kwa Mtume SAAW na masahaba wake.

Na lau Uislamu ungekuwa dini ya kiroho tu kama vile unavyohubiriwa na baadhi leo basi wakina Abuu Jahali na wenzake wasingekuwa na sababu ya kupambana na Uislamu, kwani Mtume SAAW hakuwahi kattu kuabudu masanamu na makuraishi hawakumfanyia uadui kwa hilo. Hii ikiwa ni dhahiri uadui

Inaendelea Uk 6

KUNUFAIKA NA NAJISI

Swali:

Je inafaa kuchukua jeni ya nguruwe kwa mfano jeni ya ukuaji na kuiweka katika chakula halali mfano matango kwa ajili ya ukuaji..?



Kuchukua jeni za ngurue, kuziweka kwenye mimea ili kuongeza ukuaji wake, kama vile kuzitumia katika ukuaji wa matango na vyenginevyo, hili halifai. Na ni kwa sababu ya dalili zifuatazo:

-Nguruwe ni haramu na ni najisi kwa dalili zifuatazo:

"Mumeharamishiwa nyamafu, damu, nyama ya ngurue, na kili-chochinjwa si kwa ajili ya Allah..." TMQ Maida: 3

-Ametoa Tabarani katika *Al-Kabiir* kutoka kwa Abi Tha'alaba Al-Khushani, amesema: Nilimwendea Mtume (SAW) nikamwambia ewe Mjumbe wa Allah: Na mimi nipo kwenye ardhi ya *ahlulkitaab* na wao wanakula katika vyombo vyao nguruwe na wananywea ulevi, je nile katika vyombo hivyo na ninywe...? Kisha Mtume (SAW) akasema: *"...na ukipata vyombo vyengine, usile katika vyombo vya makafiri na kama hukupata basi vikoshe hivyo (vya makafiri) kwa maji sana, kisha kulia humo"*, yaani ukivihitaji na ukiwa hukupata vyengine, vikoshe vizuri, haya yanatoa dalili kuwa ulevi na nguruwe ni najisi kwa kuwa vinahitaji kukoshwa ili kuvitahirisha. Na katika riwaya ya Daruqutny anataja Mtume (SAW) kuvikosha kwa maji ndio tohara yake ni dalili ya wazi juu ya unajisi wa nguruwe na ulevi. Na hii hapa riwaya ya Daruqutny: kutoa kwa Abi Idris, kutoka kwa Al-Hushany amesema: Nilimwambia

Ewe Mjumbe wa Allah SAAW hakika sisi tunachanganyika na washirikina na hatuna vyungu wala vyombo vyengine visivyokuwa vyao : Akasema:

سَتَنُغْنُو عَنْهَا مَا اسْتَطَعْتُمْ فَإِنْ لَمْ تَجِدُوا فَارْحُصُوهَا بِالْمَاءِ
فَإِنَّ الْمَاءَ طَهُورٌ ثُمَّ اطْبَحُوهَا فِيهَا

"Jitengeni navyo kadri muwezavyo, kama hamkupata (vyengine), vikosheni kwa maji, kwani hakika ya maji ndio tohara yake, kisha vipikieni". Hii ni *nass* ya wazi kwamba ulevi na nguruwe ni katika najisi, kwani Mtume (SAW) anasema:

"Hakika ya maji ndio tohara yake".

-Ametoa Bukhar kutoka kwa Jabir ibn Abdillah (RA), hakika yake amemsikia Mtume (SAW) akisema katika mwaka wa Ufunguzi wa Makkah na yeye yuko Makkah:

"Hakika Allah na Mjumbe wameharamisha kuuza ulevi, nyamafu, nguruwe, masanamu, pakasemwa ewe Mjumbe wa Allah waonaje shahamu ya nyamafu kwani hupakwa kwenye marikebu, na hupakwa kama mafuta kwenye ngozi, na watu hutumia kama nishati ya kuwashia, akasema hapana, hiyo ni haramu, kisha akasema Mjumbe wa Allah (SAAW) awaangamize Allah mayahudi hakika Allah ali-poharamisha shahamu yake (nyamafu) wao wakaitengeneza vizuri kisha wakaiuza wakala kipato chake (thamani)"

-Na akatoa Muslim kutoka kwa Ibn Abass, amesema, Umar ilimfikia kuwa Samura ameuza ulevi, akasema: Allah amuangamize Samura, kwani hajui kwamba Mjumbe wa Allah (SAW) amesema: *"Allah amewalani mayahudi wameharamishiwa shahamu wao wakaitengeneza vizuri kisha wakaiuza"*.

-Na ametoa Abu Daud kutoka kwa Abi Huraira, kwamba Mjumbe wa Allah (SAW) amesema: *"Hakika Allah ameharamisha ulevi na thamani yake, na ameharamisha nyamafu na thamani yake, na ameharamisha nguruwe na thamani yake"*.

Dalili hizi zinabainisha uharamu wa kunufaika na najisi, kwahiyo, haifai kuchukua jeni kutoka nguruwe na kuiweka kwenye mimea ili kuongeza ukuaji wake. Wala hapasemwi hakika hii ni kama dawa ambayo inafaa kutumia najisi pamoja na kuwa karaha, kwa yale aliyoyapokea Bukhar kwa njia ya Anas (RA): ..

"Hakika watu kutoka Uraina waliuchukua mji, Mjumbe wa Allah akawaruhusu wende kwa ngamia wa sadaka wanywe maziwa yake na mkojo wake..." Hapasemwi hivyo kwasababu kukuza mimea hakuwi katika maana ya neno dawa. Kwa hivyo, haifai kutumia jeni kutoka nguruwe ili kukuza mimea.

Allah ni Mjuzi

Ndugu yenu Atta Ibn Khalil Abu Al-Rashtah

Amiri wa Hizb ut Tahrir

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPPC), David Kafulila alisiki-ka akihusisha ongezeko la watu na shinikizo katika matumizi ya rasilimali za taifa. Alisema kuwa kasi kubwa ya ongezeko la watu nchini ni miongoni mwa changamoto zinazoathiri ukuaji wa uchumi na kiwango cha kipato cha mtu mmoja mmoja..

Akizungumza katika mhadhara wa Umma uliofan- yika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) Jumatano, Juni 3, 2026), Kafulila amesema Tan- zania ina wastani wa ongezeko la watu unaozidi asilimia 3 kwa mwaka.

Kulingana naye Tanzania ina- kabiliwa na ukuaji mkubwa wa idadi ya watu wa asilimia 3.4% kwa mwaka, kiwango ambacho kinazidi wastani wa Afrika (2%). Pia alidai kuwa kuna haja ya kudhibiti uzazi (uzazi wa mpango) ili rasili- mali zilizopo zitumike kwa ufanisi wakati nchi ikijiinua kiuchumi.

Kama haitoshi bwana Kafulila alisisitiza kuwa mbali na kudhibiti idadi ya watu, kuna haja ya kuwekeza kwenye afya na maarifa ili kuwajenga wananchi kuwa wazalishaji bora.

Hoja kwamba idadi kubwa ya watu ndio chanzo cha umasiki- ni ni hoja dhaifu na ni muen- delezo wa nadharia ya kibepari (Malthusianism) ina- yojaribu kukimbia kiini halisi cha tatizo. Umasikini hausaba- bishwi na idadi ya watu wala



uchache wa rasilimali, bali unato- kana na mfumo mbovu wa ugawaji wa rasilimali, udhaifu wa mfumo wa kiuchumi, usimamizi usio na thabiti nk. Watu wengi sio mzigo, bali ni nguvu kazi, uzalishaji na soko.

Tatizo halisi lipo katika maeneo ya- fuatayo:

1. Mfumo Mbovu wa ugawaji wa rasilimali na utajiri

Tatizo kuu la kiuchumi kilimwen- gu sio ukosefu wa mali, bali ni urundikaji wa utajiri mikononi mwa watu au makampuni machache. Mfumo wa sasa una- poruhusu rasilimali za Umma kama madini, nishati, na ardhi ku- binafsishwa na kumilikiwa na ma- bepari wachache au makampuni hasa ya kigeni kutoka nchi za kibepari kama za Ulaya ya ma- gharibi na Amerika.

Matokeo ya hilo wananchi wengi wanabaki bila fursa bali humalizia unyone na ufukara. Ukifuatilia takwimu utaona Tanzania kwa mwaka inasafirisha kiasi cha tani 48-60+ zenye thamani ya mabilioni ya dola ambazo zinaweza kutatua mambo mengi lakini zinakua na mabepari wachache.

2. Utegemezi wa Mfumo wa Riba na Madeni ya Nje

Nchi nyingi zinazoendelea zime- fungwa kwenye mtego wa madeni kutoka taasisi za mabepari ambazo

kwa hakika zipo chini ya Ma- rekani na Uingereza ambazo zimepewa jina za kimataifa ka- ma IMF na Benki ya Dunia na mashirika ya ukopeshaji kama Paris club na mfano wake. Hizi zimeandaa mfumo usiokwepe- ka kwa kuzifanya nchi changa kama Tanzania kutumia sehemu kubwa ya mapato yao ya ndani kulipia riba na marejesho ya madeni badala ya kuwekezwa kwenye miundombinu ya uzalishaji, elimu, afya nk.

3. Mfumo wa Fedha na Mfu- muko wa Bei (Fiat Money)

Utumiaji wa fedha za karatasi zisizo na hifadhi ya dhahabu au fedha unadhoofisha nguvu ya kununua ya wananchi. Ma- bepari kupitia mfumo wao mpya wa fedha wa dola umesababisha kila siku thamani ya fedha ya ndani kushuka, wananchi maskini ndio wanaoumia zaidi, bila kujali idadi yao katika nchi ni ndogo au kubwa. Hili limekuja baada kuondosha mfumo wa fedha za madini, yaani dhahabu au fedha (gold & silver standard) na kuwekwa fedha ya karatasi am- bayo sio thabiti.

4. Kutotumia vyema Nguvu Kazi (Human Capital)

Idadi kubwa ya watu ni fursa ya kiuchumi. Kushindwa kwa serikali au mfumo wa kiuchumi kutengeneza mazingira ya vi- wanda, kilimo cha kisasa, na teknolojia ili kuajiri nguvu kazi hiyo ndiko kunakozalisha ukosefu wa ajira na umasikini, sio uwepo wa watu wenyewe. Na hili linahakikishwa na

Inaendelea uk 8

wao uliibuka katika muktadhaa wa kupingwa sera zao za kisiasa, uchumi, utawala nk.

2. Kwa Wanaopinga sherehe za mazazi ya Mtume SAAW

a.Amma wapingao maulidi nao wanaangukia mule mule katika makosa ya kukaza misuli katika mambo yenye ikhtilafu ki-sheria na kulegeza misuli katika mambo ambayo uwajibu wake hauna ikhtilafu.

Mfano, yupi awezaye kusema kulingania Uislamu kama mfumo wa maisha sio wajibu? Bali utawaona kundi hili wao wamechagua Sunna mbili tatu na kuzifanya ndio bakora ya kuwachapia Waislamu ambao hawajajifunga na Sunna hizo, ilhali Waislamu wengine nao wamejifunga na Sunna zingine.

b.Kuona uharamu wa sherehe za maulidi ni dhambi kubwa kuliko Umma wa Kiislamu ulivyowatupa mkono Waislamu wa Palestina, Yemen, Sudan, Kashmiri nk. japo hata kwa dua. Huku kundi hili lipingalo maulidi wakitetea watawala wa nchi za Kiislamu kwa kutopeleka majeshi yao kunusuru Waislamu, bali hata maswaibu ya nayowagusa Waislamu wa mae-neo yetu ya karibu, wao hawana uchungu nayo labda yakigusa wa-fuasi wao.

c. Kukataa kwamba jambo hili halina ikhtilafu, kwa hoja kuwa Mtume SAAW hakufanya, huku na wao wakifanya ambayo Mtume SAAW hakufanya kama sherehe za tahfidhi Quran nk.

d. Kuunga kwao mkono tawala ambazo zinagongana na aqida ya Kiislamu na wakihimiza zipendwe zitiwe na zienziwe, ilhali aqida

waliyoibeba ya Kiislamu inakataa misimamo hiyo. Kwani aqida ya Kiislamu haiwezi kuunga mkono itikadi inayosema Allah Taala hana nafasi katika maisha ya siasa, utawala, uchumi, jamii nk.

Ni matarajio makubwa kwamba Umma wa Kiislamu utazibeba nasaha hizi kwa ikhlasi na uchamungu na kuzifanyia kazi, ambapo kazi kubwa, ya wajibu na nyeti inayotukabili kufanya ulinganizi wa kurejesha tena maisha ya Kiislamu kwa kurejesha dola ya Kiislamu ya Khilafah.

Afrika50 ... Kutoka uk 1

wa miundombinu barani Afrika kupitia fedha kutoka sekta ya umma na sekta binafsi, ndani na nje ya Afrika.

Kama ilivyo kwa mashirika mengine ya kikanda, kibara na kimataifa, Africa50 licha ya kuwa ni chombo cha kikoloni, kamwe kama zilivyo taasisi nyingine za aina hiyo, haiwezi kuleta maendeleo bora na ya kweli kwa Afrika.

Pamoja na taasisi ya Africa50 ku-shiriki katika miradi mbalimbali ya miundombinu, kama vile awamu ya kwanza ya mradi wa gesi asilia (LNG) nchini Tanzania, chini ya Shirika la Tanzania Petroleum Development Corporation (TPDC) kwa ku-shirikiana na TAQA Arabia, kuhusika katika uendelezaji wa usafirishaji wa umeme kupitia Shirika la Umeme Tanzania (Tanzania Electric Supply Company), kushirikiana na Wizara ya Afya ya Tanzania katika kuongeza uwezo wa nchi ili kusaidia uwekezaji katika miundombinu ya afya, vifaa tiba na uwezo wa uendes-haji wa muda mrefu, lakini ukitazama kwa makini utagundua kuwa Africa50 si chochote zaidi ya

jukwaa na chombo cha kuwezesha ajenda za kikoloni na unyonyaji wa nchi za magharibi, zinazowasilishwa kwa jina la "washirika wa Maendeleo."

Kwa mfano, Shirika la British International Investment (BII) limefanya uwekezaji wa dola milioni 20 za Marekani katika "Africa50 Infrastructure Acceleration Fund"(IAF), na hivyo kuifanya BII kuwa mshirika muhimu zaidi wa mfuko huo. Hatua hiyo imefanya jumla ya uwekezaji katika mfuko huo kufikia takribani dola milioni 330. Aidha, BII imesaini Mkataba wa Makubaliano (MoU) na Africa50 kwa lengo la kubaini fursa za uwekezaji wa pamoja, ufadhili na uhamasishaji wa mitaji katika miradi ya miundombinu barani Afrika.

Hili ni dalili ya wazi kwamba jukwaa la Africa50 si chochote zaidi ya mkono wa ukoloni unaolenga kuin-yonya Afrika kwa kisingizio cha kuendeleza miundombinu.

Zaidi ya hayo, kwa mujibu wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), inakadiriwa kuwa pengo la ufadhili wa miradi ya miundombinu barani Afrika linafikia hadi dola bilioni 108 kwa mwaka, licha ya juhudi zilizofanyika kwa zaidi ya muongo mmoja.

Upungufu wa fedha za ku-gharamia miundombinu barani Afrika unaonyesha kuwepo kwa mfumo wa utegemezi wa kikoloni. **Inaendelea Uk 8**

Kufungiwa na kukamatwa kwa mabilioni ya dolari katika akiba ya benki kuu, kuwekwa kwa vikwazo vya kiuchumi, ukiukwaji wa uhuru wa anga ya Afghanistan, na kampeni kubwa ya propaganda dhidi ya maadili ya Kiislamu yote yanaendelea kwa nguvu zote. Kwa hivyo, kutoka kwa mtazamo wa kisheria wa Kiislamu, kuanzisha uhusiano wowote wa kidiplomasia, kisiasa, au kiuchumi na "dola yenye uhasama" ambayo mikono yake imejaa damu ya Waislamu ni batili na ni haramu.

Kwa upande mwingine, kuyaalika makampuni ya Marekani na serikali ya Marekani kuchimba madini ya Afghanistan na kupata udhibiti wa miundombinu yake kunaleta maafa mawili.

Kwanza, dola za kibepari za Magharibi zimekuwa zikiziona ardhi dhaifu kama mawindo ya kuporwa. Sera hii ya uwindaji ilidhihirishwa kikamilifu katika makubaliano ya hivi karibuni kuhusu Ukraine, ambapo msaada wa Marekani ulihusishwa na kupata udhibiti na usimamizi wa rasilimali za madini, mafuta, na gesi, na hivyo kupelekea aina ya "kukamatwa kwa mali ya mtindo wa kikoloni."

Pili, madini na maliasili za ardhi za Waislamu ni mali ya Ummah na lazima zitumike kwa maslahi na nguvu ya Waislamu na kwa ajili ya kudhihirisha Dini. Kwa kuwa madini ya kimkakati yana dori muhimu katika viwanda vya makombora, mifumo ya rada, na teknolojia za ulinzi na kijeshi, kukabidhi rasilimali hizi

muhimu ni sawa na kusaidia kudumisha nguvu ya kikoloni ya Amerika, kudhoofisha Waislamu, na kuimarisha upanga wa adui anayezitumia kutengeneza makombora na mabomu ambayo kisha huangushwa juu ya watu waliokandamizwa wa Gaza, Lebanon, na nchi zengine za Kiislamu.

Waziri wa mambo ya nje wa Afghanistan pia alikuwa amesema hapo awali kwamba: *"Ninaamini uwezo wa Rais Trump wa kufanya mikataba, mbinu yake ya kivitendo, na uamuzi wake ni mambo ambayo yanaweza kuwezesha ushirikiano mzuri na utawala wake."* Dhana kama hiyo kuhusu wanasiasa wa Marekani, haswa Donald Trump, inagongana kabisa na mtazamo wa Kiislamu. Mtazamo wa Trump kuhusu ulimwengu ni wa umiliki na wa kikoloni. Anaendelea kuwa na matarajio ya kuchukua udhibiti wa Kambi ya Anga ya Bagram, anaunga mkono unyakuzi kamili wa Palestina, na sasa anazungumzia kwa ukali kutangaza Mlango-Bahari wa Hormuz kuwa sehemu ya eneo la Marekani.

Je, unasisitiza kuendelea ku-shirikiana kwa karibu na mtu ambaye sio tu anaupiga vita Uislamu kivitendo, lakini pia anatangaza uadui wake waziwazi kwa maneno pia? Wakati wa muhula wake wa kwanza wa urais, Trump alitangaza waziwazi: *"Tutaunganisha ulimwengu uliostaarabika dhidi ya ugaidi mkali wa Kiislamu, ambao tutauondoa kabisa kutoka kwenye uso wa Dunia."*

Kwa hivyo, badala ya kuweka matumaini yako katika dola za kikoloni za Magharibi na kuingia katika mikataba nazo, nyoosheni mkono wa udugu kwa Waislamu—marafiki zenu wa kweli—wanaowaita kuelekea chanzo cha heshima ya kweli: kusimamishwa upya kwa Khilafah Rashida ya Pili kwa Njia ya Utume.

Wito huu wa kweli, tofauti na siasa za vitendo za Magharibi, sio muamala wa kibiashara au kiuchumi; badala yake, ni muamala mtukufu na Mwenyezi Mungu (swt). Kutoa nusra kwa dawah hii kutakuongozeni kwenye heshima, nguvu, na nafasi ya uongozi duniani, kama vile Uislamu ulivyowahi kuwainua Waarabu waliogawanyika na waliokuwa wajinga kutoa pembezoni mwa historia hadi nafasi ya uongozi na amri ulimwenguni.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْكَافِرِينَ أَوْلِيَاءَ
مِنْ دُونِ الْمُؤْمِنِينَ أَلْيُؤَدُّونَ أَنْ تَجْعَلُوا لِلَّهِ
عَلَيْكُمْ سُلْطَانًا مُبِينًا

"Enyi mlio amini! Msiwafanye makafiri kuwa ndio marafiki badala ya Waumini. Je, mnataka Mwenyezi Mungu arwe na hoja iliyo wazi juu yenu?" [Surah An-Nisa: 144]

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tah-
rir
katika Wilayah Afghanistan**



Inakadiriwa kuwa mahitaji ya miundombinu ya bara yanafikia zaidi ya dola bilioni 170 kwa mwaka, wakati kwa hali ya sasa ni takriban dola bilioni 80 tu ndio zinazotengwa kwa ajili ya miundombinu kila mwaka, ambapo ni takriban asilimia 40 pekee inayotokana na serikali za Afrika. Fedha zilizobaki zinatoka katika mataifa ya kikoloni na taasisi zao za kifedha za kikoloni.

Afrika inaweza kutatua tatizo la miundombinu ikiwa kusengekuwepo na unyonyaji wa kikoloni wa rasilimali zake, ambazo zinakadiriwa kuwa na thamani ya dola trilioni 29.5. Afrika ina takriban asilimia 40 ya dhahabu yote duniani, asilimia 90 ya platinamu na kromiamu, na zaidi ya asilimia 50 ya kobalti na manganizi, pamoja na asilimia 65 ya ardhi yote inayofaa kwa kilimo ambayo bado haijalimwa duniani.

Rasilimali hizi zote, pamoja na nyingine nyingi, zinanufaisha

zaidi mataifa ya kikoloni, huku bara la Afrika likiachwa katika umaskini uliokithiri usioelezeka, likiwa na miundombinu duni au kutokua nayo kabisa.

Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), ambayo ndio taasisi mama ya jukwaa la miundombinu la Africa50 kama ilivyo kwa taasisi nyingine za kifedha za kibepari, hutoza viwango vya juu vya riba kwa mikopo inayotoa kwa mataifa ya Afrika kwa ajili ya kugharamia mahitaji yao ya miradi ya miundombinu.

Kiuhalisia, Afrika inanyongwa si tu na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia (WB), bali pia na mikopo ya miundombinu inayotolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika inayodaiwa kuwa ni taasisi nyumbani (ya kiafrika). Mikopo hiyo inaongeza zaidi mzigo wa madeni ambao tayari ni mzito na usiovumilika kwa mataifa ya Afrika.

Katika Uislamu, ujengaji wa miundombinu ni sehemu muhimu ya ustawi wa wananchi, jambo ambalo hufanywa na Dola ya Khilafah kwa kutumia hazina yake (Bayt al-Māl). Hazina hiyo itakua na mapato ya kutosha, kwa kuwa ulimwengu wa Kiislamu una rasilimali na utajiri wa kutosha.

Mara Khilafah Rashidah itakaporejeshwa, taasisi zote za kikoloni za kibepari zenye unyonyaji, pamoja na taasisi zao za kifedha, zitatimuliwa katika ardhi zetu na kunyimwa kabisa fursa ya kushiriki katika ujengaji wa miradi yote.

Imeandikwa na Said Bitomwa

Mjumbe wa Afisi ya Habari Hizb ut Tahrir Tanzania

Kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir

Idadi ya watu. Inatoka uk 5

madola makubwa kwa kutupatia na kutupangia elimu ambayo ni ya nadharia zaidi. Angalia kichekesho ! eti ili mtu awe rubani lazima asomee physics au hesabu, kitu ambacho hata mtoto ana uwezo wa kukijua bila elimu yeyote. Isitoshe fani hiyo imewekewa gharima kubwa kujifunza.

5. Ukoloni Mamboleo na Mikataba Isiyo ya Haki

Maliasili ghafi na rasilimali nyingi

za nchi changa zinaendelea kusafirishwa kwenda nje kwa bei ya kutupwa, huku nchi zikirejesha bidhaa zilizosindikwa kwa bei ya juu sana. Unyonyaji huu wa kibishara unazinyima nchi fursa ya kujenga thamani ya ndani (value addition).

Kwa hiyo, msingi wa tatizo sio watu kuwa wengi, bali ni tatizo la kimfumo, ambapo leo mashaka yote husababishwa na mfumo wa

kibepari. Ili tuweze kuondosha matatizo yanayomkabili mwanadamu ni kwa kuweka mfumo bora kabisa wa Kiislamu ambao una nidhamu mwanana ya kiuchumi ambayo hudhamini usambazaji wa rasilimali zilizoenea kwa uadili fu kuondoa dhiki, umaskini na mashaka kwa wanadamu.

Ali Amour

Mjumbe wa Afisi ya Habari-Hizb ut Tahrir Tanzania